**SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA(HALMASHAURI ZA WILAYA)**

**(SURA NA. 287)**

**SHERIA NDOGO**

**Zimetungwa chini ya kifungu cha 160.**

**SHERIA NDOGO ZA MAMLAKA YA MJI MDOGO WA SAME. (USAFI,AFYA NA MAZINGIRA) ZA 2013**

Jina na tarehe ya kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitajulikana kama Sheria Ndogo za Mamlaka ya Mji Mdogo Same ( Ada na Ushuru) za mwaka 2013 na zitaanza kutumika mara baada ya kutangazwa katika gazeti la Serikali.

Eneo la kutu-Mika

2. Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote lililopo chini ya Mamlaka ya Mji Mdogo Same.

3. Katika Sheria Ndogo hizi, isipokuwa kama zitatafsiriwa vinginevyo na Sheria nyinginezo:-

**"Ada ya kuondoa taka"** ina maana kiwango cha fedha kilichowekwa na Mamlaka ya Mji Mdogo kulipia gharama za kuzoa taka kama ilivyofafanuliwa na sheria ndogo za Mamlaka ya Mji Mdogo Same (Ada na Uhuru);

**"Afisa Mwidhiniwa"** ina maana ya mtumishi wa Mamlaka aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelezwa vinginevyo;

**"Afisa Mtendaji Mkuu"** ina maana ya Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Mji Mdogo Same pamoja na Afisa yeyote aliyeteuliwa kwa wakati huo atakayekuwa akikaimu nafasi ya Afisa Mtendaji Mkuu;

**"CBO"** maana yake ni kikundi cha kijamii kinachoundwa kwa ajili ya kutatua tatizo au kufanya shughuli ya maendeleo katika jamii ya eneo hilo ambapo CBO imeundwa.

**"Eneo la kiutawala"** maana yake ni eneo lote lililopo ndani ya mipaka ya Mamlaka ya Mji Mji Mdogo Same;

**"Eneo lililozuiwa"** maana yake ni maneo yote yaliyoko chini ya Mamlaka ya Mji Mdogo ambapo majani marefu na mimea

imepigwa marufuku kuwepo na inahusisha maeneo ya wazi, mitaa na barabara;

**"Kampuni"** Taasisi au chombo chochote kilichosajiliwa chini ya Sheria ya Makampuni sura ya 212;

**"Leseni za biashara"** ni kibali cha maandishi cha kuruhusiwa kufanya biashara au shughuli yoyote;

**"Machinjio"** maana yake ni sehemu iliyotengwa na Mamlaka kwa ajili ya kuchinjia wanyama, kuanika ngozi za wanyama waliochinjwa machinjioni;

**"Nyumba za vyakula"** maana yake ni hoteli, baa, mgahawa, magenge ya vyakula, mama lishe, vibanda vya kahawa na inajumuisha mahali popote ambapo ni maalum kwa uuzaji wa vyakula aina yoyote;

**"Mamlaka"** maana yake ni Mamlaka ya Mji Mdogo Same;

.

**"Makazi"** inamaana nyumba, ghorofa au jengo lolote linalo tumiwa kwa kuishi, pia inajumuisha ardhi ambayo haijaendelezwa lakini imetolewa kwa ajili ya nyumba za kuishi.

**"Matangazo ya biashara"** ni ishara, alama, maneno, au kitu chochote chenye kuashiria kuijulisha jamii juu ya uwepo wa shughuli ya kuuza na kununua;

**"Masoko"** ni sehemu yoyote iliyotengwa na Mamlaka ya Mji Mdogo Same kwa ajili ya kuuza na kununua vitu;

**"Mitaa"** maana yake ni mitaa midogomidogo iliyo katika Mamlaka ya Mji Mdogo Same.

**"Mzabuni"** maana yake ni mtu au kikundi cha watu au makampuni yaliyoidhinishwa na Mamlaka kufanya kazi zote kama atakavyoelekezwa na Mamlaka.

**SEHEMU A. USAFI.**

4. – (1) Afisa yeyote aliye idhinishwa na Mamlaka ya Mji Mdogo atakua na uwezo wa kukagua eneo lolote lililopo chini ya Mamlaka ya Mji Mdogo Same kwa nia ya kuangalia kero na kutoa maelezo ya kuondoa kero hizo.

(2) Maafisa hao ni Afisa Mtendaji Mkuu pamoja na watendaji

wake na inajumuisha pia Wenyeviti wa Mitaa na Watendaji ya Kata.

5. – (1) Nimarufuku mtu yeyote kuweka au kutupa taka, mchanga au uchafu wowote utakaoleta chukizo katika mtaa, uchochoro au eneo lolote lililokatazwa na Mamlaka.

(2) itakua ni kosa kukiuka au kwenda kinyume na kifungu cha 5 (1) cha sheria ndogo hizi.

6. – (1) Mtu yeyote anayemiliki nyumba au mpangaji wa nyumba anatakiwa kuweka chombo cha kukusanya taka chenye ukubwa unaotosheleza na kiwe na mfuniko unaofaa na kinatakiwa kitumike kilasiku katika nyumba hio

(2) ukusanyagi wa taka ngumu utafanywa na Mamlaka au mtu yeyote aliyeidhinishwa na Mamlaka kufanya kazi hio kwa niaba ya Mamlaka na ada ya uzoaji taka inatozwa kulingana na sheria ndogo za Ushuru na Ada za mwaka 2005.

(3) kulingana na kifungu cha 6 (1) (2) cha sheria ndogo hii ni marufuku kwa mtu yeyote kuweka katika chombo cha kuhifadhia taka au maji machafu kitu chochote ambacho kinaweza kuleta madhara kwa binadamu au kusababisha moto.

(4) Takataka zote zihifadhiwe ndani ya ua mpaka hapo zitakapochukuliwa na Mamlaka au mwenye nyumba au mpangaji kuzipeleka mwenyewe kwenye maeneo maalumu yaliyo tengwa.

7. Mmiliki wa nyumba au mpangaji wa nyumba atalazimika kutunza takataka zilizohifadhiwa kwenye pipa la taka au chombo chochote kinachokubalika kisheria hadi hapo Mamlaka au mtu yeyote aliyeteuliwa na Mamlaka kuzichukua na kuzuitupa jalalani.

8. - (1) Ni jukumu la mwenye nyumba au mpangaji kuweka chombo cha kuhifadhia taka katika nyumba yake ili kuwezesha ukusanyaji wa taka hizo kwa rahisi.

(2) kila mwenye basi litakalo ingia eneo la Mamlaka atawajibika kuwa na chombo cha kuhifadhia taka na kuhakikisha kwamba kila abiria anatupa taka katika chombo hicho.

(3) itakua ni kosa kwa mwenye basi au dereva au kondakta iwapo abiria aliyeko ndani ya basi lake atatupa kitu chochote barabarani au katika kituo cha basi.

(4) mwenye basi au dereva au kondakta atawajibika kulipa faini ya shilingi elfu thelathini baada ya kujazwa fomu ya ilani na afisa wa Mamlaka.

9. Ni marufuku kwa mtu yeyote kumwaga takataka au kuzichoma moto ovyo bila idhini ya Mamlaka.

10. Mwenyenyumba au mpangaji anatakiwa kukata majani yasizidi kimo

cha sm. 15 na kukata uzio na kuondoa mabaki na kuyaweka kwenye chombo ch kuhifadhia taka au sehemu iliyoruhusiwa kuhifadhi taka hizo.

11. Ni marufuku mtu yeyote kumwaga, kutiririsha maji taka kwenye mtaa katika mataa, uchoro, eneo la wazi, mtaro ulio wazi au mashimo yasio ruhusiwa.

12. Utakua ni wajibu wa mwenye nyumba kuunganisha choo cha maji na uchafu wake kwenye mtaro wa maji taka, iwapo atashindwa kufanya hivyo atatakiwa aelekeze uchafu huo katika mashimo ya maji taka yaliyo kubaliwa na Mamlaka.

13. - (1) Ni marufuku mtu yeyote kuchafua au kuvuruga maji yanayotumika na binadamu au mnyama.

(2) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuoga au kufulia kwenye chanzo cha maji, mto au mfereji au tangi halikuwepo kwa madhumuni hayo.

14. Endapo kutatokea kero zinazosababishwa na maji taka katika nyumba yenye mpangaji zaidi ya mmoja na iwapo mwenye nyumba hawezi kupatikana kwa haraka, Mamlaka inaweza kuamuru wapangji kufanya lolote linalowezekana ilimkuondoa na gharama hizo zitafidiwa na kodi watakayo mlipa mwenye nyumba.

15. - (1) Endapo Mamlaka itagundua kwamba nyumba inayokaliwa na watu vyoo vyake vipo katika hali ya uchafu.

(2) Mtu yeyote anayemiliki jengo au inayotumika kama makazi anatakiwa aweke vyoo vya kutosha kama Mamlaka itakavyoona inafaa.

(3) Mtu yeyote anayemiliki kiwanda, shule mgahawa, shule za bweni, hoteli au jengo lolote la umma, sehemu za burudani, au nyumba yeyote atatakiwa kuweka vyoo vinavyoridhisha kwa ajili ya matumizi ya wanaume na wanawake na atahakikisha vyoo hivyo vina mwanga na hewa ya kutosha

(4) Ni marufuku mtu yeyote kuendesha biashara ya nyumba ya wageni au hosteli bila ya kibali cha Mamlaka

(5) Kibali cha hosteli ya wanafunzi au nyumba ya wageni kitatolewa kwa kuzingatia yafuatayo:-

a. Mwanga na hewa ya kutosha
b. Nafasi
c. Vifaa (samani) vya kutosha
d. Uimara wa jengo
e. Uondoshaji wa maji taka, taka miminika na taka ngumu
f. Usafi wa jumla wa majengo na vifaa vyake na
g. Utoshelezaji wa vyoo / bafu kwa jinsia yote.

(6) Kila mgahawa wa vyakula au vinywaji ni lazima pawe na

vyoo vya kutosha kwa ajili ya
wateja, watumishi na wapiti njia

(7) Hairuhusiwi kufunga milango ya vyoo kwa kufuli la aina yeyote ile.

(8) Atayepatikana kufunga mlango wa choo kwa kufuli ili kuzuia wapita njia wasitumie vyoo atawajibika kulipa faini isiyoTsh. 30, 000/= papo kwa hapo.

16. Choo cha aina yeyote ambacho kwa maoni ya Mamlaka kitaoonekana kutumika kichafu au kuhatarisha maisha ya binadamu, hakitaruhusiwa kutumika mpaka hapo Mamlaka itakaporidhika na matengenezo choo yaliyofanyika.

17. Ni marufuku kwa mtu yeyote kuchimba au kujenga shimo kwa ajiliya kuhifadhi kinyesi au maji taka bila idhini ya maandishi iliyotolewa na Mamlaka.

18. Ni marufuku kwa mtu yeyote kutupa kinyesi, makopo, mate au matapishi katika uchochoro, mtaani au eneo lolote lisiloruhusiwa.

19. - (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kuendesha kiwanda hicho kinachotoa maji taka bila ya kuwa na mitambo ya kusafishia maji taka hayo ambayo imeidhinishwa na Mamlaka.

(2) Kwa maana hiyo ni marufuku mtu yeyote kuruhusu maji taka kutoka viwandani, au eneo lolote linalofanya utengenezaji kuingia katika vyanzo vya maji safi, ardhini, maeneo wazi, mitambo ya maji taka, uchochoro, mitaro iliyowazi kabla ya kuyasalimisha kwa kiwango kinachokubalika naMamlaka.

(3) Kila baada ya miezi mitatu kabla na baada ya kusafisha maji taka kutoka viwandani yatatakiwa kupimwa kuangaliwa ubora wake na maabara ya Serikali au maabara yoyote iliyoruhusiwa na Serikali na majibu au matokeo ya uchunguzi huo kuletwa Mamlaka.

20.- (1) Ni marufuku mtu yeyote kusababisha au kuruhusu eneo la nyumba anayoishi kuwepo uchafu wa takataka au majani yoyote marefu.

(2) Itakuwa ni wajibu mmiliki mpangaji wa nyumba kufagia na kuondoa uchafu au malundo ya uchafu na kuweka safi eneo la mbele la nyumba yake.

(3) Itakuwa ni wajibu wa mwenye nyumba kutunza sehemu ya nyuma ya nyumba yake kwa kutotupa taka pia kuondoa taka, na nyasi ndefu.

(4) Vichochoro vyote vitatunzwa na wenye nyumba husika na kila mwenye nyumba/mpangaji atawajibika kutunza eneo linaloangukia kwake yaani kila nyumba itakuwa na kujisehemu katika uchochoro huo kwa mujibu wa Sheria.

21. - (1) Ni marufuku kwa mtu yeyote kutelekeza magari mabovu kwenye njia ya miguu, mtaa au vichochoro au mitaro iliyo wazi na kusababisha adha kwa wakazi au watumiaji wa njiia hiyo.

(2) Ni marufuku mtu yeyote kutengeneza au mtambo eneo ambalo sio mahususi kwa shughuli hiyo au eneo lisiloruhusiwa na Mamlaka.

22. - (1) Mamlaka au mtu yeyote aliyeteuliwa kama wakala atakuwa na uwezo wa kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha na kutupa taka za majumbani na biashara kwa kulipa kama ilivyoainishwa katika Sheria ndogo ya Ada na Ushuru ya mwaka 2005.

(2) Kamati za Maendeleo za Mitaa na Kata zitakuwa na uwezo chini ya Sheria hii kusimamia usafi kwenye maeneo yao kwa kukomesha utupaji taka ovyo na usafishaji wa vichochoro.

(3) Kamati za Maendeleo za Kata na Mitaa zitakuwa na uwezo wa kumtoza yeyote atakayechafua mazingira kwa namna yoyote ile faini isiyozidi shilingi elfu kumi.

(4) Iwapo mchafuzi wa mazingira hakuwa na fedha ya kulipa pindi anapokamatwa, Kamati husika itawajibika kukamata mali yake yenye thamani kama hiyo fedha.

(5) Fedha zitakazopatikana kwa njia hii zitatumika kwenye shughuli za maendeleo za Mtaa au Kata husika na ni lazima zikatiwe stakabadhi rasmi ya Kata au Mtaa husika.

(6) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kumzuia mjumbe wa Kamati ya maendeleo ya Kata au Mtaa kutimiza matakwa ya sheria.

(7) Kama hana fedha wala mali apewe adhabu ya kusafisha kwa kadri mamlaka/Kata/Mtaa utakavyoona inafaa.

23. Kila mkazi kwenye nyumba au mpangaji kwenye nyumba ya makazi nyumbani atawajibika kuweka chombo cha kuridhisha cha kuweka taka za majumbani chenye ujazo unaoridhisha na chenye mfuniko unaofaa na kuhakikisha kuwa takataka zote zinazozalishwa kwenye nyumba hiyo zinawekwa humo kila siku. Mradi chombo hicho kiwe kinatosheleza kuweka taka zote. Takataka hizo zitatolewa nje pindi gari la kuzisomba linapopita au kupelekwa kwenye ghuba za taka zilizopo mitaani.

24. - (1) Kila mkazi kwenye nyumba ya biashara au mpangaji atalazika kuweka chombo cha kuridhisha cha kuhifadhi taka za biashara chenye ujazo wa kuridhisha na mfuniko wa kubana na kuhakikisha kuwa taka zote zinazozalishwa zinahifadhiwa kwenye chombo hicho na ujazo wake utosheleze kwa siku.

(2) Mamlaka kama itakavyoona inafaa itaelekeza sifa za chombo hicho na ujazo wake utosheleza kwa siku.

(3) Itakuwa ni kosa kwa mtu yeyote kukiuka matakwa ya kifungu

kidogo cha 24 (1) na atiwapo hatiani atawajibika kulipa faini ya shilingi Elfu hamsini au kwenda gerezani kwa kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja faini na kifungo.

25.- (1) Hairuhusiwi mtu au kikundi cha watu kubomoa jengo lolote kwa nia yoyote ile bila kupata kibali cha Mamlaka kwanza.

(**2) Kila anayetaka kubomoa nyumba atatakiwa kuomba kibali cha kubomoa nyumba na kutoa malipo ya awali kabla ya kubomoa. Malipo hayo ni kwa ajili ya gharama za kuondoa vifusi na mabaki ya kubomoa kwa kadri itakavyokuwa imetathminiwa na Mamlaka.**

3) Mtu yeyote anayetaka au kukarabati jengo lolote atatakiwa kuhifadhi vifusi na vifaa vingine vya ujenzi ndani ya eneo au kiwanja chake na sio barabarani au kwenye hifadhi ya barabara.

26. - (1) Kila mwenye nyumba na mtumiaji wa sehemu ambapo taka za viwandani zinazalishwa kwa malundo au taka za hospitali au taka zozote zinapozalishwa atapaswa kuzitunza taka hizo na kuhakikisha kuwa anaziondoa kwa usanifu wa kuridhisha au jinsi atakavyoelekezwa mara kwa Mamlaka.

(2) Mamlaka itatoza ada za uzoaji taka kwa biashara zote kulingana na ukubwa wa uzalishaji kwenye makazi, taka hatari na maeneo mengine kama Mamlaka itakavyoona inafaa.

(3) Mtu yeyote atakayevunja Sheria ndogo hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika atapewa adhabu ya faini isiyozidi shilingi elfu hamsini (50, 000/=) au kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja kifungo na faini, vile atatakiwa kurejesha gharama za uharibifu atakaokuwa amesababisha.

(4) Itakuwa ni kosa mtu yeyote kuweka mtambo au mashine au gari, pikipiki n.k. inayochafua hewa kwa kutoa moshi mzito au mwingi unaosababishwa na uchakavu wa chombo chenyewe.

27. - (1) Kila mmiliki/mkazi wa nyumba ya mkazi au biashara atawajibika kuweka taka zote azalishazo mahali atakapoelekezwa na Mamlaka hii, iwapo mtu yoyote atashindwa kufanya hivyo atakuwa ametenda kosa.

(2) Mtu yeyote atakayevunja Sheria Ndogo hii atakuwa ametenda kosa na ikithibitika kuwa ametenda kosa atapigwa faini isiyopungua shilingi elfu thelasini (30, 000/=) na isiyozidi elfu hamsini (50, 000/=) au

kifungo cha miezi kumi na mbili au vyote kifungo pamoja na faini.

28 - (1) Mamlaka itaweka mipango na utaratibu wa ukusanyaji na utupaji taka kutoka kwenye sehemu za biashara na nyumba za kuishi na kuzizoa taka hizo na kuzitupa.

(2) Mamlaka inaweza kufanya kazi ya kukusanya taka yenyewe au kuteua Wakala kwa makubaliano maalum.

29. - **(1) Mzalishaji yeyote, mfanyabiashara au mchuuzi wa mazao au vitu vinavyoharibika au kuoza kwa haraka sokoni vitu hivyo vikiwa vimefungwa au kufunikwa kwa majani, majani ya miti au aina nyingine yoyote ya sehemu ya mmea.**

(2) Itakuwa halali kwa Afisa mtendaji Mkuu au mtu mwingine aliyeidhinishwa kuelekeza aina ya chombo kitakachopendekezwa kutumika kupakia mazao au vitu vinavyoweza kuharibika iwapo mazao hayo yatakiwa kuletwa ndani ya eneo la Mamlaka ya Mji Mdogo na kila mzalishaji au mfanyabiashara au mchuuzi atalazimika kufuata maelekezo hayo.

(3) Mamlaka kadri itakavyoona inafaa inaweza kusitisha uingizaji au kulazimisha kutolewa kutoka kwenye masoko aina yoyote ya mazao au vitu vinavyoharibika ambavyo hufungwa na kupakiwa kama ilivyo kwenye kifungu cha 29 (1) cha Sheria Ndogo hii.

30. - (1) Kila mfugaji wa ng'ombe, mbuzi, kuku, nguruwe na wanyama wengine wa nyumbani atawajibika kukusanya na kuhifadhi uchafu wowote utokanao na wanyama hao kama vile kinyesi, manyoya, utumbo (baada ya kuchinjwa) na uchafu utokanao na ufugaji huo mfano nyasi au mabaki ya vyakula vyao katika hali ambayo itairidhisha Mamlaka na ambayo haitaleta kero kwa jamii.

(2) Kila atakayetaka kufuga wanyama waliotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) ni budi awe na eneo la kutosha.

(3) Hairuhusiwi kabisa kufuga aina yeyote ya wanyama wanaotajwa kwenye kifungu kidogo cha (1) kwenye eneo la msongamano wa makazi.

(4) Kwa namna yoyote ile ufugaji ni lazima uwe na mnyama kuwa pahala pamoja.

31. Ada yoyote ya kuzoa taka inavyoanishwa katika Sheria Ndogo hizi itakuwa ni deni kwa Mamlaka au wakala wake na inaweza kudaiwa kutoka kwenye kaya au mmiliki kwa mujibu wa sheria.

(1) Madeni ya ada ya kondoa taka iliyoainishwa kwenye kifungu cha 31 yatakusanywa kutoka kwa mmiliki kwa kumpelekea Hati ya Madai kwa maandishi na iwapo atashindwa kulipa kwa muda wa siku 14, Mamlaka au mtu yeyote aliyeidhinishwa anaweza kufungua kesi ya madai Mahakamani au kukamata mali ya mdaiwa yenye thamani ya kiasi anachodaiwa.

32. Mali iliyokamatwa kwa jinsi hii itauzwa kwa mnada wa hadhara iwapo mhusika hataikomboa ndani ya siku ishirini na moja (21) tangu siku iliyokamatwa.

(1) Baada ya uthibithisho wa Afisa mtendaji Mkuu au Afisa aliyeidhinishwa juu ya deni lenyewe na kuhakikisha kuwa mmiliki hajalipa licha ya kupelekewa madai mahakamani, itathibitisha hayo na hiyo itakuwa Hati ya idhini ya kutekeleza hukumu dhidi ya madai hayo

kwa njia yoyote ile na itakuwa sawa na idhini ya kukamata mali na idhini ya kuuza mali iliyokamatwa, sawa na inayotolewa na mahakama hiyo kwenye kesi nyingine za madai.

33. Kila shahada inayopelekwa katika Mahakama kama ilivyo kwenye sheria ndogo ya 32 itakuwa ni kielelezo cha kweli cha kuonyesha maelezo yaliyotolewa na sahihi.

34. - (1) Isipokuwa pale ambapo sheria andishi nyingine inaeleza vinginevyo, Afisa Mtendaji Mkuu anaweza kufuta leseni ya biashahara ambapo mmiliki mwenye biashara atakaposhindwa kuonyesha stakabadhi ya kulipia ada ya taka.

(2) Kabla ya kufuta leseni hiyo Mamlaka au Afisa aliyeruhusiwa atatakiwa atoe ilani ya maandishi ya siku zisizopungua kumi na nne kueleza nia ya kufanya hivyo kwa kumtaka mhusika alipe ada hiyo mara moja.

35. Ada itatakiwa kulipwa siku thelathini baada ya mmiliki , mpangaji au mfanyabiashara kupata taarifa.

36. Mamlaka inaweza kumteua mtu yoyote kukusanya ada na kuzoa taka na inaweza kuingia naye mkataba wa kufanya kazi za ukusanyaji na uzoaji taka ikiwa ni pamoja na kumpa uwezo wa kumpeleka Mahakamani mtu yoyote anayeshindwa kulipa ada ya ukusanyaji au uzoaji taka kwa mujibu wa sheria ndogo hii.

37. - (1) Iwapo kero itaonekana mahali au makazi kwasababau ya biashara au taka za majumbani kutupwa eneo la makazi Mamlaka itampa ilani mmiliki au mkazi anayeishi kwenye nyumba hiyo na kutaka aondoe
kero hiyo kwa mda utakaotakiwa kwa mandashi.

## SEHEMU B.

## WAHUDUMU KUTHIBITISHWA AFYA ZAO.

30 (1). Wahudumu wote wanaohudumia katika biashara za vyakula na vinywaji ikiwa ni pamoja na hotel, mikahawa, mashine za kusaga nafaka, baa, pamoja na huduma nyinginezo zinazofanana na hizo atalazimika kupima afya pamoja na kujisajili kwa Afisa Mtendaji Mkuu wa Mji.

(2) Pasipokuathiri kifungu cha 20 (1) cha Sheria Ndogo hii, muhudumu atalazimika kupima na kuthibitishwa afya yake na tabibu wa afya katika hospitali ya wilaya.

(3). Ada ya kupima na kuthibishwa afya kwa mhudumu italipwa kama itakavyoonyeshwa katika jedwali la sehemu “**A**” la sheria Ndogo hii.

**SEHEMU C.**

UTEUZI NA MAMLAKA YA WAKALA

31. (1). Mamlaka inaweza kumteua mtu yeyote au kikundi chochote kuwa wakala wa kusimamia usafi, mazingira, kuikusanya ada na ushuru mbalimbali kama ilivyoonyeshwa katika Sheria ndogo za Ada na Ushuru za Mamlaka ya Mji Mdogo.

.

(2). Wakala anaweza kutumia mamlaka atakayopewa na Mamlaka ya Mji Mdogo Same kumfungulia shitaka la madai Mahakamani dhidi ya mtu au kikundi chochote kitakachoshindwakuweka mazingira safi, kulipa ada na shuru, chini ya Sheria Ndogo hizi.

**SEHEMU D.**

MAKOSA

32. Mtu yeyote au wakala ambaye bila sababu ya msingi: -

(a) Atashindwa kutoa maelezo anayotakiwa kama ilivyoelekezwa chini ya Sheria Ndogo hizi.

(b) Atashindwa kuwasilisha makusanyo au kulipa ada au, ushuru au vyote;

(c) Atashindwa kutunza kumbukumbu au taarifa kuhusu ada na na leseni inayotolewa na Afisa Biashara au Afisa muidhiniwa.

(g). Atajenga au kufanya maendelezo ya kiwanja chake ndani ya Mamlaka bila kuwa na idhini ya maandishi ya Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlakai au afisa muidhiwa.

33. Ni kosa kumzuia, kumshawishi na kufanya fujo wakati afisa wa afya au afisa yeyote wa Mamlaka, anapotekeleza wajibu wake chini ya Sheria ndogo hizi.

34. Pasipokuathiri kifungu cha 15 cha Sheria Ndogo hii, mtu yeyote atakayetumia matangazo ya biashara yake, kumtukana, kumdhalilisha au, kumfedehesha mtu au biashara ya huyo mtu kwa namna yoyote ile, atakuwa anafanya kosa chini ya Sheria Ndogo hii.

35. Mtu yeyote atakayevunja mojawapo ya kifungu/vifungu vya she - ria ndogo hizi, na akakiri kwa maandishi mbele ya Afisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka au Afisa yoyote muhidhiniwa, Afisa Mtendaji

Mkuu ana haki ya kutoza faini isiyozidiTshs. 100, 000/= (Mia moja Elfu tu) sambamba na gharama nyinginezo amabazo Mamlaka ime - Gharimu kukabiliana na kosa hilo.

36. Mtu yoyote, Kampuni au Shirika lolote, litakalovunja au kukiuka Mojawapo ya kifungu katika Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda Kosa na Mamlaka ikimtia hatiani, atatozwa faini isiyozidi Tsh. 300, 000/= ( Mia tatu eltu tu) au kifungo kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au vyote kwa pamoja.

**JEDWALI.**

**ADA YA USAJILI WA WAHUDUMU**

Kutakuwepo na ada kwa ajili ya usajili wa wahudumu

| S.NO | AINA YA ADA | KIASI | MUDA |
|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya usajili wa mhudumu | Tshs. 2, 000/= | Kwa mwaka |
| 2 | Hati ya kuandikishwa | Tshs. 1, 000/= | Kila baada ya miezi sita |
| 3 | Ada ya kupima afya | Tshs. 1, 000/= | Kila baada ya miezi sita |

Muhuri wa Halmashauri ya wilaya Same umebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio lililopitishwa kwenye Mkutano wa Halmashauri uliofanyika tarehe ………… Mwezi ………………………………………2013 na kubandikwa mbele ya: -

…………………………………………………
J. Mkude.
**Mkurugenzi Mtendaji(W.)**

…………………………………………
IRIRA C.M.
**Mwenyekiti Halmashauri ya Wilaya.**

**NAKUBALI**

**……………………………………**

**LEONIDAS T. GAMA.**

MKUU WA MKOA KILIMANJARO

Tarehe……..................2013